Kumbuka: Si kila mgonjwa wa kifua kikuu ana VVU na si kila anayeishi na VVU ana kifua kikuu

Huduma shirikishi za kifua kikuu na VVU ni zipi?

- Mgonjwa wa kifua kikuu na mtu anayehisiwa kuwa na kifua kikuu anashauriwa na kupimwa VVU
- Mgonjwa wa kifua kikuu na aliyegundulika ana VVU ataanzishiwa dawa za kupunguza makali ya VVU na dawa ya kuzuia magonjwa nyemelezi
- Mtu anayeishi na VVU huchunguzwa kama ana kifua kikuu ili aanzishiwe dawa za kutibu kifua kikuu na kama hana atapewa dawa za kuzuia
- Mgonjwa wa kifua kikuu atapewa ushauri wa namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU

Matibabu ya kifua kikuu:

- Kifua kikuu kinatibika pale mgonjwa anapozingatia maelekezo na taratibu wa matibabu
- Dawa za kutibu kifua kikuu hutolewa chini ya utaratibu wa usimamizi wa umezaji dawa kila siku.
- Msimamizi wa dawa hizo anaweza kuwa mfanyakazi wa afya au mwanajamii aliyefundishwa kufanya hivyo.
- Ni muhimu mgonjwa akamilishe kumeza dawa kwa kipindi chote alichopangiwa ili apone kabisa.
- Matibabu ya kifua kikuu cha kawaida yanachukua muda wa kuanzia miezi 6-12 kulingana na aina ya kifua kikuu
- Matibabu ya kifua kikuu sugu yake ni miezi 12 -24

Matibabu ya UKIMWI

- Hadi sasa hakuna dawa za kutibu virusi vya UKIMWI, zipo dawa za kupunguza makali ya UKIMWI, ambazo huboresha kinga ya mwili na kumfanya mgonjwa arejee kuendelea na shughuli zake kama kawaida.
- Dawa za kupunguza makali ya VVU zinatumika kwa muda wote wa maisha ya mtu anayeishi na VVU mara baada ya kuanza kuzitumia.

Mgonjwa mwenye magonjwa ya kifua kikuu na UKIMWI kwa pamoja hutibiwa katika kliniki ya kifua kikuu mpaka anapomaliza matibabu ya kifua kikuu kisha kuendelea na matibabu ya kupunguza makali ya UKIMWI katika kliniki ya VVU

Dawa za kifua kikuu na kupunguza makali ya UKIMWI hutolewa bila malipo katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za serikali, mashirika ya kidini na hospitali binafsi

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

World Health Organization

END TB TANZANIA

The Global Fund



FAHAMU UHUSIANO KATI YA KIFUA KIKUU NA UKIMWI

Kifua Kikuu ni nini?

Kifua kikuu ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea aina ya bakteria visivyoonekana kwa macho ya kawaida bali kwa kutumia hadubini. Kuna aina mbili za kifua kikuu; kinachoshambulia mapafu na nje ya mapafu kama mifupa. Kifua kikuu cha mapafu ndio chanzo cha maambukizi.

Mtu anaambukizwaje kifua kikuu?

Mtu anambukizwa kifua kikuu kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa wa kifua kikuu ambaye hajaanza tiba, anapokohoa au kupiga chafya hutoa vimelea ambavyo husambaa kwenye hewa na iwapo mtu mwingine asiye na ugonjwa huu akivuta hewa hiyo anaweza kuambukizwa.

Dalili za kifua kikuu ni zipi?

Dalili za kifua kikuu ni pamoja na:

- Kukuhoa kwa wiki mbili au zaidi
- Kukohoa makohozi yenye mchanganyiko wa damu
- Kutoka jasho kwa wingi hasa wakati wa usiku hata maeneo ya baridi
- Kupata homa za mara kwa mara wakati wa jioni kwa wiki mbili au zaidi
- Kupungua uzito

Kumbuka: Ukikohoa wiki mbili au zaidi mfululizo wahi kwenda kwenye kituo cha huduma za afya kwa uchunguzi

Virusi vya UKIMWI (VVU) ni nini?

Ni vimelea aina ya virusi vinavyo shambulia kinga ya mwili na kusababisha ugonjwa wa UKIMWI.

UKIMWI ni nini?

Neno UKIMWI ni kifupisho cha Upungufu wa Kinga Mwilini. VVU vinapoingia katika mwili wa binadamu hushambulia chembe chembe nyeupe za damu hivyo kusababisha mwili kukosa kinga yake ya asili dhidi ya magonjwa. Mwili ukipungukiwa na kinga ya asili hushambuliwa kwa urahisi na magonjwa nyemelezi.

Mtu anaambukizwaje VVU?

Zipo njia kuu tatu za maambukizo ya VVU:

- Kujamiana na mtu anayeishi na VVU bila kutumia kondomu
- Maambukizi kutoka kwa mama mwenye VVU kwenda kwa mtoto wakati wa ujauzito, kujifungua na kunyonyesha
- Kwa njia ya damu yenye maambukizi: kama kuongezewa damu, kushirikiana vifaa vyenye ncha kali kama vile: nyembe, sindano, mikasi na visu vya kutogea, kukeketa, kukata kimeo ambavyo havijasafishwa vizuri.

Dalili za UKIMWI ni zipi?

Dalili za UKIMWI ni pamoja na:

- Homa za mara kwa mara
- Mwili kuwa mchovu, maumivu ya misuli.
- Kuumwa na kichwa
- Utando mweupe mdomoni na midomo kukauka
- Upele mwilini (unaowasha)
- Kikohozi cha mara kwa mara kwa zaidi ya mwezi mmoja
- Mkanda wa jeshi au wengine huita moto wa Mungu (malengelenge)
- Kuharisha mara kwa mara
- Mwili kupungua uzito
- Kuugua magonjwa nyemelezi ikiwa ni pamoja na:
- Kifua kikuu
- Homa ya mapafu (pneumocystis pneumonia)
- Saratani

Kuna uhusiano gani baina ya Kifua Kikuu, VVU na UKIMWI?

Kifua kikuu na UKIMWI ni magonjwa mawili yenye uhusiano ambapo kila ugonjwa huongeza kasi ya ugonjwa mwingine.

Mtu anaweza kuishi na vimelea vya Kifua kikuu bila kuugua kifua kikuu kama kinga yake ya mwili ni imara.

- Mtu anayeishi na VVU kinga yake ya mwili inapopungua husababisha vimelea vya Kifua
- kikuu kuanza kushambulia mwili na kusababisha ugonjwa wa Kifua Kikuu.
- Mtu anayeishi na VVU ni rahisi kuambukizwa na kuugua kifua kikuu kwani kinga ya miili yao hupungua
- Kifua kikuu huharakisha mtu anayeishi na VVU kuugua UKIMWI
- Kifua kikuu ni ugonjwa nyemelezi unaoongoza
  kusababisha vifo kwa watu wanaoishi na VVU
- Mtu anayeishi na VVU ana uwezekano mkubwa wa kupata kifua kikuu sugu